

MUHTASARI WA SERA YA USTAHIKI WA KUPOKEA USAIDIZI WA KIFEDHA

NANI ANAWEZA KUTUMA OMBI:

Sera ya ustahiki wa kupokea usaidizi wa kifedha inatoa punguzo la hadi 100% kulingana na pato la kaya kwa wale ambao wamejaribu mbinu nyingine zote za malipo, na

- Wana pato lisilozidi 250% ya Miongozo ya mwaka huo ya Umaskini ya Serikali Kuu.
- Wamewasilisha ombi la usaidizi wa kifedha lililojazwa kabisa.

Washauri wa Kifedha wapo ili wakusaidie kujaza ombi la usaidizi wa kifedha. Pia wanaweza kukuadia kujisajili kwa bima kupitia Masoko ya Bima ya Afya.

JINSI YA KUTUMA OMBI:

- Wewe mwenyewe katika jengo lolote la Huduma za Afya ya Kiakili za Kikristo za Pine Rest (Pine Rest) pamoja na bewa kuu, ambalo liko katika anwani hii:

Pine Rest Christian Mental Health Services
300 68th Street SE
Grand Rapids, MI 49548
- Kwa kutuma ombi kwenye MyChart
- Kwa kupiga simu kwenye idara ya Akaunti za Wagonjwa ya Pine Rest:

1-616-455-5019
- Kwa kutembela dawati la maelezo au ofisi ya mapokezi katika kituo chochote cha Pine Rest.
- Kwa kwenda kwenye:
[pinerest.org/financial assistance](http://pinerest.org/financial%20assistance)
- Kwa kumtumia barua pepe Mshauri wa Kifedha kwa anwani:
patientaccounts@pinerest.org

ILI KUPATA NAKALA ZA BILA MALIPO ZA SERA HII NA OMBI:

- Tumia maelezo ya mawasiliano yaliyoorodheshwa hapa juu.
- Nakala kwa lugha nyingine zitatolewa baada ya kuagiza.

Watu wanaohitimu hawatatozwa ada kwa huduma za dharura au zinazohitajika kimatibabu na hawatawekewa bili inayozidi viwango jumla vinavyotozwa kwa huduma za dharura na nyingine zinazohitajika kimatibabu.